unywe." Yesu alikuwa amezungumzia kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu maishani mwetu. Yesu ndiye mpeanaji. Ni ya bure. Njoo ukielewa na kutambua hitaji lako na kujua kwamba namna ulivyo si bora vya kutosha. Biblia huita hali hiyo toba, kusema unahuzunikia kile ulichofanya kibaya maishani na kutoweza kumtumainia Mungu, ili kuweza kupokea msamaha kutoka kwake na makosa yote kuondolewa. Tunapokuwa huru kutoka kwa yote tuliokuwa kinyume na Mungu maishani mwetu, tunampokea Yesu Kristo na Roho wa Mungu. Tunabadilishwa, tunazaliwa tena, tunaingia kwa ufalme wa Mungu, tunaona ufalme wa Mungu na mara tunaelewa kwamba Mungu ametupenda siku zote. Anatupenda na tunaweza kuendelea kwa upendo wake maishani mwetu.

Yesu aliomba kwamba upendo aliokuwa nao kutoka kwake uwe ndani yetu. Upendo uliofanya Yesu awe jinsi alivyokuwa ndani yetu. Mwishowe, Yesu anamwambia Nikodemu kile ambacho kimekuwa kifungu cha kujulikana sana kwa bibilia "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee ili yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele" "yeyote" inamaanisha kwamba yeyote atakayependa.

Unaweza kumpokea Bwana Yesu leo na upate kujua mabadiliko ya ajabu katika maisha yako ambayo Yesu ameahidi.

Kwa msaada na mashauri, wasiliana nasi kwa**:**
contact@revivalUK.org.uk

## OMBI LA WOKOVU

Unaweza kuomba ombi hili kutoka moyoni ombi lako kwa uaminifu kwasababu anakupenda.

Mpendwa Bwana Yesu.

Asante kunisaidia wakati sikuweza kujisaidia. Ninaungama kwako kwamba nimetenda dhambi na kufanya vitu kinyume na mapenzi yako. Tafadhali nisamehe na unitakase kutoka kwa dhambi zangu zote. Tafadhali njoo moyoni mwangu na unibadilishe ili niweze kukutumikia kwa ukweli maishani mwangu. Natambua pasipo wewe, sinatumaini ulimwenguni lakini nikiwa na wewe ninao uzima wa milele. Bwana Yesu ninakushukuru. Sasa mimi ni wako na ninafurahi ndani yako kama mwokozi wangu na naweza kukuita Bwana sasa kwa ukweli.

Amina.

kama unajua unamwitaji Bwana Yesu awe mwokozi. Atajibu

Produced by revivalUK
www.revivalUK.org..uk
contact@revivaluk.org.uk

Kuzaliwa Tena

MISSIONARY FELLOWSHIP OF KENYA

# " KUZALIWA TENA"



www.revivalUK.org.uk

# Kuzaliwa Tena

## KUZALIWA TENA

**M**semo huu hutumika kwa mtu yeyote ambaye amefanya uhuisho wa ajabu ama ameanzisha kitu kipya maishani.”Born again bikers”, kwa mfano humaanisha wazee wa kike kwa wakiume ambao wakati mmoja katika ujana wao waliendesha baiskeli na tena wanarudia kuendesha katika miaka zao za hamsini ama sitini.Msemo huu husemwa kutoka kwa bibilia na kwa hivyo tutazame na tuone maana yake zaidi.

Katika injili ya Yohana, mtu mwenye elimu na masemo ya juu, Nikodemu, anamjia Yesu na maswali kadhaa. “Wewe hufanya miujiza hufanyazo usifanyazo namna gani?, kuna kitu tofauti sana kukuhusu,ni kitu gani? Yesu hajibu swali kwa njia ile Nikodemu alitarajia lakini akamwambia “unahitaji kuzaliwa mara ya pili ikiwa utauona ufalme wa Mungu” Yesu alijua vile miujiza zilitendeka waziwazi na alitaka kumuonyesha Nikodemu kitu bora zaidi. Maskini Nikodemu hakuelewa,”Itanibidi tena nirudi tena tumboni mwa mama yangu?”Yeye aliona vitu kutoka kwa mtazamo wa kiasili.Kisha akamwambia anahitaji kuzaliwa katika roho ikiwa ataingia katika ufalme wa Mungu (Mtu huweza tu kuona ufalme wakati anaingia ndani) Kuzaliwa tena kiroho kulihitajika, “kile kilichozaliwa kwa mwili ni mwili na kile kilicho zaliwa kwa roho ni roho,Yesu akamwambia.

Yesu baada ya ufufuo wake pia alizungumza na mtume Petro kuhusu kuzaliwa tena. Yesu alitumia maneno, “ukibadilishwa”,magari, kwa mfano yanaweza kubadilishwa yatumie mafuta tofauti kwa kuendeshwa. Chanzo cha nguvu zake ni tofauti.Shida ya Nikodemu alijuwa kwamba kile alicho kuwa katika kuzaliwa kwake kwa kiasili hakikuwa kizuri. Maisha ya Yesu na kazi yake ilikuwa kwa sababu alizaliwa kwa roho wa Mungu. “Nikodemu unahitaji uwe kama mimi kiroho kisha utaelewa jinsi ya kuishi na kumtumikia Mungu”.

Sisi zote lazima tutambue kwamba namna tulivyo kiasili si bora vya kutosha. Mtume Paulo, mmoja wa wanadini mwenye masomo cha juu alifikia uamuzi kwamba hakukuwa na chochote kizuri ndani mwake. Alihitaji msaada apate kubadilika. Kisha alifurahi kwamba Mungu alipeana njia ya yeye kubadilika. Anatumia msemo mgumu ingawaje anaeleza kimaakini kile Mungu alimfanyia, “Sheria ya roho ya uzima katika Kristo Yesu ameniweka huru kutoka kwa dhambi na mauti.”Wakati Paulo alimpokea Bwana yesu, sheria mpya ya kiroho, ukipenda kanuni, alikuwa ameingia katika maisha ya Kristo na ilikuwa imemweka huru kutoka kwa sheria ya kiroho ya kale ambayo ilikuwa imefanya kazi maishani mwake kabla ya Yesu kumbadilisha. Alikuwa amezaliwa tena. Alikuwa huru kwa vile alikuwa, na sasa alienenda katika upya wa uzima. Hii ni hali sawa na ile ambayo Yesu alikuwa anamweleza Nikodemu kwamba mwanzo mpya wa kiroho, kuzaliwa kupya; hakuna haja ya kurudi tumboni mwa mama yake ila hitaji ni la kumpokea maishani mwako asema Yesu.

Furaha ni kwamba mabadiliko haya yanapatikana kwetu sote. Yesu alipokufa msalabani alifanya kuzaliwa kupya kuwezekana kwetu. Bibilia inasema “Mungu alikuwa ndani ya Kristo Yesu akipatanisha ulimwengu wote kwake.” Ni msemo mgumu kwako lakini hivyo ndivyo ilivyotendeka.

Tunampokea Bwana Yesu namna gani? Hili ni swali ambalo Nikodemu labda angeuliza ama alitaka kuuliza mara ya kwanza. Labda alikuwa mwoga sana kuuliza na ndivyo kwa sababu aliuliza swali alilouliza. Alitambua waziwazi alihitaji kubadilika baada ya kujua kwamba hakukuwa bora vya kutosha na kwamba alikuwa tofauti. Hakuwa amewahi kukutana na mtu kama Yesu hapo awali.

Hapo ndipo sote tunaanzia, kwa kutambua kwamba hata tuwe wazuri, werevu, wasomi, tajiri, wakujulikana na yale ambayo tunaweza kuwa na kuwaza, hiyo sio nzuri ya kutosha. Tunamhitaji Yesu kutubadilisha. Yeye ndiye mwenye uzima, uzima ule wa kiroho ambao zote tunahitaji. Nikodemu alielewa haya, kwa hivyo akamjia Yesu, ambaye alikuwa kile alichohitaji.

Siku nyingine, mwisho wa sherehe katika Israeli, Yesu alipasa sauti, “Ikiwa yeyote anaona kiu,” Ni ya kushangaza kwa sababu utaelewa kwamba wote walikuwa wamekunywa vya kutosha na hawangeona kiu wala kuwa na njaa. Lakini hii ni kiu ya kiroho na njaa ya kiroho. Je, kila kitu hukuacha utupu ulimwenguni?

Yesu alisema ”Ikiwa una kiu, njoo kwangu na